102/3
Kiswahili
Karatasi ya 3
Fasihi
July/ August 2016
Muda: Saa: 2 ½

MTIHANI WA PAMOJA WA SUKEMO
Kenya Certificate of Secondary Education
KISWAHILI
Karatasi ya 3
FASIHI
Muda; saa 2 ½

MAAGIZO:

a) Jibu maswali **manne** pekee.
b) Swali ya **kwanza** ni la **lazima**.
c) Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobakia yaani ,Riwaya, Tamthilia; Ushairi na Fasihi Simulizi.
d) Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.
e) Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
f) Karatasi hii ina kurasa **5** zilizopigwa chapa.
g) Watahini wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SWALI LA LAZIMA.

SEHEMU YA A – HADITHI FUPI

DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE – KEN WALIBORA

1) Shaka ya mambo

"Basi itakuwa bado mapema."
"Hapana, n' na mengi ya kufanya kabla ya kukutana na … kabla ya miadi yangu. Basi usichelewe."

(a) i) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii) Huku ukitumia hoja **tatu** , jadili umuhimu wa huyo aliyekuwa anaenda 'kukutana' naye. (alama 6)

Ndoa ya Samani

(b) "Hadi leo, sitaki kusikia lolote kumhusu Amali na ndoa yake ya samani."

Eleza sababu **kumi** kwa nini msemaji wa kauli hii hataki kusikia lolote kumhusu Amali. (alama 10)

SEHEMU YA B – RIWAYA

KIDAGAA KIMEMWOZEA – KEN WALIBORA

Jibu swali la 2 au 3

2) " … unatukanisha ukoo wetu … naona aibu kukuita ndugu yangu … Hii ni aibu bwana …"
(a) Jadili muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Tambua mbinu kuu ya lugha katika dondoo hili kisha uieleze. (alama 2)

(c) Kwa kurejelea riwaya nzima, tambua na ueleze matumizi mengine **saba** ya mbinu uliyotaja (b) hapa juu. (alama 14)

AU

3) "Lowela tunapendana mno na ni msiri wangu wala hakuogopa kuniambia yaliyojiri."

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

(b) Fafanua 'yaliyojiri' kwa mujibu wa dondoo hili. (alama 4)

(c) Lowela ni kielelezo kibaya cha msichana wa kisasa. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea riwaya yote ya Kidagaa Kimemwozea. (alama 12)

SEHEMU YA C – TAMTHILIA

MSTAHIKI MEYA – TIMOTHY AREGE

Jibu swali la 4 au 5

4) "Karibu tunastaafu lakini hakuna hazina maana hakuna cha kuweka…. Ni kazi ya kijungu jiko."

(a) i) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

ii) "Kazi tunayoifanya ni ya kijungu jiko." Kwa kurejelea tamthilia hii thibitisha kwa kutumia hoja **sita**madhara ya Wanacheneo kufanya kazi ya kijungujiko. (alama 6)

(b) Je, wananchi wa Cheneo walifanya nini ili kuboresha maisha yao. (alama 10)

AU

5) "Fahamu hili. Anayeliogopa tope kumwangukia hawezi kujua njia nzuri ya kulisafisha …"

(a) Kwa nini msemewa anaogopa tope kumwangukia? (alama 4)

(b) Jadili jinsi uongozi mbaya unavyoathiri pakubwa mji wa Cheneo. (alama 16)

SEHEMU YA C – USHAIRI

Jibu swali la 6 au 7

6) Soma shairi hili kisha ujibu maswali.

Nilikuomba chakula, nawe kweli kaninyima
Sikuwa hata na hela, kakimbila kwenye **dhima**
Megunduwa ewe Shilla, hunijalingi daima.

Sisahau kisogoni, mnobe ulipokuwa
Makabadhi linombeni, nani kwa wema litowa
Na libasi za mwilini, samani za mtakawa.

Shilla ya shule **sifutu**, lokufanyia hisani
Dafutari na madutu, sare pia likupeni
Linisumbua kuntu, na mie kavumileni

Kozi na nilikupeni, kulipa karo chuoni
Ulinisapa kamani, mnobe nikabakini
Asante punda yani, ni mateke wajamani

Bada ya kazi mwanangu, siku ‘tupa abadani.
Nilisaka msenangu, lodi rafiki moyoni
Ka ‘pa kazi wanguwangu, hela nyingi kushikeni

Babayo alifariki, ukiwa bado kiini
Kiacha bila rafiki, hapo hapo pa nyumbani
Nami amiyo kacheki, na nikakuchukueni

Waringa kama tausi, wewe Shilla ni kinyonga
Daraja usilitusi, lokuvusha engaenga
Unapofika ofisini, kumbuka kutojitenga

Maswali

(a) Lipe shairi hili anwani inayofaa. (alama 1)

(b) Bainisha hisani **tatu** alizofanyiwa nafsinenewa. (alama 3)

(c) Tambua nafsineni katika shairi hili. (alama 1)

(d) Andika ubeti wa **pili** katika lugha nathari. (alama 3)

(e) Taja na ueleze mbinu **tatu** alizotumia malenga ili kutosheleza mahitaji yake ya kiarudhi. (alama 3)

(f) Eleza toni za shairi hili. (alama 1)

(g) Fafanua sura ya shairi hili. (alama 3)

(h) Ainisha shairi hili ukizingatia vigezo vifuatavyo: (alama 3)
   i. Mishororo
   ii. Migao/ vipande
   iii. Vina

(i) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi. (alama 2)
   (i) dhima
   (ii) sifutu

AU

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Mwanafunzi Nifanye Nini?

Mwanafunzi: Mkufunzi wajiani, mtihani wazuzua?
Nikiona juu chini, jibu haliji sawia
Mwalimu waleta nini, jasho sisi kututoa
Mwalimu nifanye nini, mtihani wasumbua.

Mkufunzi: Pole sana mtot'angu, lakini kazana sana
Ukitaka cha mvungu, sharti inama sana
Huruma nyingi za kwangu, hazitakupa kupona
Ni mchumia kwa jua, kivulini ala.

Mwanafunzi: Mwalimu hata ni humo, lakini mambo mzungu
Nifanye nini masomo, yakae bongoni mwangu?
Bidii ypte i mumo, nilipewa naye Mungu
Mwalimu nifanye nini, mtihani wasumbua.

Mkufunzi: Na watoto pulikeni, hamushiki mashikoni
Wakati wa masomoni, mwaporomosha yoweni
Ifike mthihani, nje meno mwatoeni
Asosikia mkuu, huvunjika mguuni.

Mwanafunzi: Mwalimu sasa 'merudi, leo taenda kitali
Nyumbani siwezi rudi, baba ni simba mkali
Kosa langu hunirudi, mwalimu hata wavyeli
Mwalimu nifanye nini, mtihani wasumbua.

Mkufunzi: Nafasi ndiyo azizi, utyumie kwa faida
Wanaumia wazazi, pesangi kuwalipia
Fahari yao wazazi, ni watoto wengi pia.
Jina li bora shuleni, kadhalika na nyumbani.

Mwanafunzi: Asante sana mwalimu, masomoni takazana
Kelele ni debe mumu, kitendo husema sana
Bongo kitabu kalamu, tatumia sana sana
Walimu na wazazingu, masomoni nitapambana.

Maswali

(a) Eleza hili ni shairi la aina gani? (alama 2)

(b) Bainisha aina za urudiaji katika shairi hili. (alama 3)

(c) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 3)

(d) Eleza huku ukitoa mfano mbinu zozote **tatu** za lugha zilizotumika. (alama 3)

(e) Taja na utolee mfano **mitatu** uhuru wa kishairi uliotumika. (alama 3)

(f) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari. (alama 4)

(g) Taja toni ya shairi hili. (alama 1)

(h) Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi (alama 1)
(i) pulikani (ii) kitali

SEHEMU YA E – FASIHI SIMULIZI

7) Soma kifungu hiki kisha ujibu Maswali

(a) Mabeberu watu wabaya
Walimfunga kombozi
Nia yao ikiwa moja
Kudidimiza jamii yetu
Katika lindi la istiimari
Ela hawakufua dafu
Mabarobaro waliingia msituni
Bunduki wakashika
Kupigana kupigania wiyathi

(i) Huu ni utungo wa aina gani. (alama 1)

(ii) Fafanua majukumu **sita** ya utungo huu. (alama 6)

(b) Eleza jinsi mtambaji wa hadithi anaweza kushirikisha hadhira yake. (alama 2)

(c) Jadili njia **tatu** utakazotumia kukusanya na kuhifadhi nyimbo katika jamii. (alama 3)

(d) Fafanua sifa **tano** za ngomezi. (alama 5)

(e) Eleza maana ya istilahi hizi. (alama 3)
(i) vivugo
(ii) matambiko
(iii) vichekesho

MWISHO